

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA

Nambari ya Simu: 028-2226018
Fax Na: 028-2226128



Ofisi ya Mkuu wa (W),
S.L.P. 20,
NGARA.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. NG/D.2/2/VOL.II/64

Tarehe: 04/06/2019

Maafisa Tarafa Wote,
WILAYA YA NGARA.

Watendaji waKata zote,
WILAYA YA NGARA –Toa taarifa kwenye vijiji na vitongoji

YAH: TANGAZO KWA WANANCHI:

Ofisi ya Mkuu wa Wilaya inawatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Ngara wenye sifa zilizotajwa hapo chini watume maombi ya kujunga na Jeshi la kujenga Taifa (JKT) kwa hiari.

SIFA ZA MWOMBAJI NI HIZI ZIFUATAZO:-

1. Awe raia wa Tanzania
2. Umri
 - a. Kwa vijana wenye elimu ya **darasa la saba** umri ni kuanzia **miaka 16** hadi **18**.
 - b. Vijana wenye elimu **Kidato cha Nne** umri usiwe zaidi ya **miaka 20**.
 - c. Vijana wenye elimu **Kidato cha Sita** umri usiwe zaidi ya **miaka 22**.
 - d. Vijana wenye elimu ya **Stashahada** umri usiwe zaidi ya **miaka 25**
 - e. Vijana wenye elimu ya **shahada** umri usiwe zaidi ya **miaka 26**
 - f. Vijana wenye elimu ya **shahda ya uzamili** umri usiwe zaidi ya **miaka 30**
 - g. Vijana wenye elimu ya **shahada ya uzamivu** umri usiwe zaidi ya **miaka 35**
3. Awe na afya njema, akili timamu na asiwe na alama yejote ya michoro mwilini (Tattoo)
4. Mwenye tabia na nidhamu nzuri, hajapatikana na hatia Mahakamani na hajawahi kufungwa.
5. Kwa vijana waliomaliza elimu ya sekondari kidato cha nne wawe waliomaliza kuanzia mwaka **2016, 2017 na 2018** wenye ufaulu ufuatao:-
 - a. Wawe wamefaulu na wawe na alama (**Points**) zisizopungua **32**.
 - b. Vijana Kidato cha Sita wawe na ufaulu wa daraja la kwanza hadi daraja la nne.
6. Awe na elimu ya msingi aliyehitimu darasa la saba
7. Awe na cheti halisi cha kuzaliwa (**Original Birth Certificate**)
8. Awe na cheti halisi cha kumaliza shule (**School Leaving Certificate**)

9. Awe na cheti halisi cha matokeo (**Original Academic Certificate/Transcript**).
10. Asiwe ametumikia Jeshi la Polisi, Magereza, Chuo cha Mafunzo au KMKM wala kuajiriwa na Idara nyingine Serikalini.
11. Asiwe amepitia JKT Operesheni za nyuma
12. Asiwe amejihuisha na matumizi ya madawa ya kulevya, bangi na yanayofanana na hayo.
13. Kwa wale wenye vipaji vya michezo mbalimbali na sanaa sifa za elimu ni sawa na zilizotajwa hapo juu.

NB: Ileweke kuwa kuingia mkataba wa kujitolea na na JKT kwa muda wa miaka 2 sio wa lengo la kujairiwa na JKT au kutafutiwa ajira Serikalini, lengo ni kutoa mafunzo ya kuwasaidia katika maisha yenu na kuwaandaa kulitumikia Taifa watakapohitajika.

Maombi yatumwe kwa: **Ofisi ya Mgambo Wilaya ya Ngara,**
S.L.P. 20,
NGARA.

Mwisho wa kutuma maombi ni **tarehe 11/06/2019** **saa 01:30 mchana**

Atakayesoma tangazo hili na amjulishe mwenzake.

Tibaijuka V.J.
KATIBU TAWALA WILAYA
NGARA

Nakala: Mkuu wa Wilaya – Aione kwenye jalada

“ Katibu Tawala (M),
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S. L. P. 299,
BUKOBA.

“ Mshauri wa Jeshi la Akiba (W) Ngara